

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

OFISI YA RAIS



TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

TAARIFA KWA UMMA KUHUSU UTEKELEZAJI WA MPANGO WA MAENDELEO KWA USTAWI WA TAIFA NA MAPAMBANO DHIDI YA UVIKO-19 KATIKA TAWALA ZA MIKOA NA MAMLAKA ZA SERIKALI ZA MITAA

1.0 UTANGULIZI

Ndugu **Wanahabari**, awali ya yote napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa Rehema kwa kutuwezesha kukutana hapa leo. Vilevile napenda kuchukua fursa hii kumpongeza Mheshimiwa **Samia Suluhu Hassan**, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa jitihada zake za kupambana na ugonjwa wa UVICO-19 zilizowezesha Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kupata Mkopo wenge masharti nafuu wa Dola za **Kimarekani Milioni 567** sawa na **shilingi trilioni 1.3** kutoka Shirika la Fedha Kimataifa (IMF) kwa ajili ya **Kampeni ya Maendeleo kwa Ustawi wa Taifa na Mapambano dhidi ya UVICO-19** ili kuchangia kufufua uchumi kwa Sekta zilizopata athari za kiuchumi kutokana na madhara ya **UVIKO- 19**.

Ndugu Wanahabari, Ofisi ya Rais - TAMISEMI imeidhinishiwa kupokea jumla ya **shilingi bilioni 535.68** kati ya fedha zote zilizotolewa kwenye mkopo huo wa masharti nafuu ambayo ni sawa na **asilimia 41.1**. Kati ya Fedha hizo **shilingi bilioni 304** ni kwa ajili ya elimumsingi, **shilingi bilioni 226.68** ni kwa ajili ya afya ya msingi na **shilingi bilioni 5.00** ni kwa ajili ya kuboresha miundombinu na mazingira ya kufanyia biashara kwa wafanyabiashara wadogo.

Ndugu Wanahabari, matumizi ya Fedha hizi zimeelekezwa kwenye maeneo ya vipaumbele vinavyogusa wananchi moja kwa moja kwa ajili ya kuwaondolea kero katika kuzifikia na kuzipata huduma za afya, elimu na uwezeshaji wananchi kiuchumi, vilevile kuwakinga dhidi ya ugonjwa wa UVIKO-19, fedha hizi zimelengwa kupelekwa katika maeneo yafuatayo:-

2.0 HUDUMA ZA ELIMUMSINGI ZITAGHARIMU SHILINGI 304,740,000,000.00

Ndugu Wanahabari,

Serikali ya Jamhuri ya Muungazo wa Tanzania chini ya Rais Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan inaendelea kutekeleza mipango na mikakati mbalimbali katika sekta ya Elimu nchini pamoja na kupambana ya UVIKO – 19 kwa wanafunzi. Idara ya elimumsingi imepokea kiasi cha shilingi bilioni **304,000,000,000**

kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu katika elimumsingi ikiwemo vyumba vya madarasa na mabweni. Fedha hizo zimelekezwa katika maeneo yafuatayo;

i. Ujenzi wa vyumba vya Madarasa 12,000 katika Shule za Sekondari

Serikali imepanga kujenga vyumba vya madarasa **12,000** vitakavyogharimu **Shilingi bilioni 240** katika shule za sekondari katika Halmashauri mbalimbali nchini kwa ajili ya kujiandaa kupokea wanafunzi wa kidato cha kwanza watakaojiunga mwezi **Januari, 2022**. Ujenzi wa idadi ya vyumba vya madarasa haya unatokana na mahitaji kulingana na idadi ya wanafunzi wanaotarajiwa kujiunga na kidato cha kwanza mwaka **2022**. Maoteo ya ufaulu kitaifa yanatofautiana kati ya Halmashauri moja na nyingine kwa wastani wa ufaulu wa kitaifa wa **asilimia 90** ya wanafunzi waliofanya mtihani darasa la saba 2021. Hivyo wanafunzi wanaotarajiwa kujiunga na kidato cha kwanza Januari 2022 ni **1,022,936** mahitaji ya vyumba vya madarasa ni **20,535** ambayo hailingani na idadi ya vyumba vya madarasa **8,535** vitakavyoachwa wazi na wanafunzi **422,403** wa kidato cha nne watakaofanya mtihani mwezi Novemba, 2021. Hivyo, uhaba wa vyumba vya madarasa 12,000. Kupitia mpango huu wa Maendeleo kwa Ustawi wa Taifa na Mapambano dhidi ya UVIKO-19, Serikali itajenga vyumba vyote vya madarasa vinavyohitajika

kwa ajili ya Kidato cha kwanza mwaka 2022. Ukamilishaji wa madarasa hayo 12,000 utawezesha wanafunzi **600,000** kupata vyumba vya kusomea na hivyo utaondoa changamoto ya upungufu wa vyumba vya madarasa kwa **asilimia 100** katika shule za sekondari.

Ndugu Wanahabari,

Gharama za ujenzi wa vyumba vyote vya madarasa zitajumuisha pamoja na ununuzi wa viti na meza **600,000**. Mikoa na Halmashauri zote nchini zitanufaika na ujenzi huu kwa kuzingatia vigezo vifuatavyo; makadirio ya kiwango cha ufaulu, idadi ya wanafunzi wanaotarajia kujeungu na kidato cha kwanza na uhaba wa vyumba vya madarasa uliopo katika kila shule. Kutohana na vigezo vilivyotumika, ujenzi wa idadi ya vyumba vya madarsa utatofautiana kati ya shule moja na nyingine.

Mgao wa madarasa haya kimkoa ni kama ulivyoonyeshwa katika **Kiambatisho namba 1**. Mikoa itakayopata fedha nyingi zaidi kutohana na wingi wa wanafunzi wanaotarajia kuingia kidato cha kwanza ni Mwanza (Madarasa 985 – shilingi 19,700,000,000); Dar es Salaam (Madarasa 743 – shilingi 14,860,000,000); Geita (Madarasa 742 – shilingi 14,840,000,000); Kagera (Madarasa 709 – shilingi 14,180,000,000); na Morogoro (Madarasa 707 – shilingi 14,140,000,000). Aidha mgao wa kila Halmashauri umeonyeshwa kwenye tovuti ya Ofisi ya Rais - TAMISEMI www.tamisemi.go.tz.

ii. Ujenzi wa vyumba vya Madarasa 3,000 katika vituo shikizi vya Shule za Msingi

Ndugu Wanahabari,

Vituo shikizi ni maeneo yanayotumika kufundishia wanafunzi wa Elimu Awali hadi darasa la tatu wanaokaa mbali na shule mama. Lengo la vituo hivyo ni kuwapunguzia umbali wanafunzi wa shule za msingi wanaotembea mwendo mrefu kufuata huduma ya elimu. Mpaka sasa kuna jumla ya vituo shikizi **1,155** katika Halmashauri **148** hapa nchini. Aidha imebainika kwamba Halmashauri **36** ambazo idadi kubwa ya Halmashauri hizi zipo katika maeneo ya Majiji, Manispaa na Miji hazina vituo shikizi vya shule.

Ndugu Wanahabari,

Kupitia mpango huu, Serikali itajenga vyumba vya madarasa 3,000 katika vituo shikizi **970** ambapo jumla ya shilingi **bilioni 60** zitatumika. Ujenzi huo utawezesha wanafunzi **135,000** kupata vyumba vya madarasa bora kwa ajili ya ujifunzaji. Ukamilishaji wa vyumba vya madarasa utakwenda sambamba na ununuzi wa madawati **45,000** ambayo yatatumiwa na wanafunzi **135,000**.

Jumla ya Halmashauri 143 zitafaidika na mpango huu katika Mikoa yote 26 ya Tanzania bara. Mgawanyo wa vyumba vya madarasa katika Halmashauri umezingatia vigezo vya; idadi ya vituo shikizi, idadi ya wanafunzi na idadi ya vyumba vya madarasa iliyopo. Vituo shikizi vya shule vyenye mahitaji makubwa

vimepewa kipaumbele zaidi kwa mfano kituo cha **Nyakanazi “B”** iliyopo Halmashauri ya Wilaya ya Geita kina wanafunzi 2,357 kimetengewa fedha za madarasa **17**. Vituo shikizi **20** havijaanza kupokea wanafunzi, hivyo serikali haitapeleka fedha za ujenzi katika maeneo hayo. Vituo shikizi **165** vina idadi ya vyumba vyatya madarasa inayolingana na mahitaji ya wanafunzi. Aidha, jumla ya vituo shikizi **185** vilivyobaki vitaingizwa katika awamu ya pili ya ujenzi wa madarasa. Mgao wa madarasa haya 3,000 ni kama ifuatavyo katika **Kiambatisho namba 2**. Mikoa iliyopatiwa fedha nyingi zaidi kutokana na wingi wa wanafunzi waliopo kwenye vituo shikizi ni; Singida (Madarasa 332 – shilingi 6,640,000,000); Tabora (Madarasa 266 – shilingi 5,320,000,000); Tanga (Madarasa 228 – shilingi 4,560,000,000) Katavi (Madarasa 224 – shilingi 4,480,000,000) na Dodoma (Madarasa 175 – shilingi 3,500,000,000). Aidha, mgao wa kila Halmashauri umeonyeshwa kwenye tovuti ya Ofisi ya Rais - TAMISEMI; www.tamisemi.go.tz

Ndugu Wanahabari,

Ujenzi wa vyumba vyatya madarasa yote **15,000** katika shule za sekondari na vituo shikizi vyatya shule za msingi utaleta manufaa mengi kwa walimu, wanafunzi na jamii kwa jumla kama ifuatavyo;

- i. Kutaondoa mrundikano wa wanafunzi darasani na hivyo kuepusha uwezekano wa kupata maambukizi ya homa kali ya mapafu UVIKO – 19;

- ii. Kutasaidia vituo shikizi kukidhi vigezo vya kusajiliwa kuwa shule za msingi na zitaangizwa katika mpango wa elimu bila malipo;
- iii. Kuwezesha wanafunzi wote waliofaulu mtihani wa darasa la saba nchini kujiunga kidato cha kwanza kwa awamu moja tu badala ya wengine kusubiri awamu ya pili na tatu;
- iv. Kupunguza utoro na mdondoko wa wanafunzi utapungua kwani wanafunzi watapata huduma bora za elimu katika maeneo jirani na mazingira yao;
- v. Walimu na wanafunzi watakuwa katika mazingira bora ya ufundishaji na ujifunzaji.

iii. Ujenzi wa Mabweni 50 kwa wanafunzi wenyе mahitaji maalumu

Ndugu Wanahabari,

Wanafunzi wenyе mahitaji maalumu wamekuwa wakikabiliwa na changamoto kadhaa ikiwemo kuishi mbali na shule zenye walimu wa taaluma ya kuhudumia wanafunzi hao. Serikali kwa kulitambua hilo, imetoa jumla ya **shilingi billion 4** kwa ajili ya ujenzi wa mabweni **50**, kila bweni litagharimu **shilingi milioni 80**. Mabweni hayo yatawezesha wanafunzi **4,000** kupata malazi bora wakati wote wakiwa shulenii.

Ujenzi wa mabweni utafanyika katika mikoa yote 26, uteuzi wa Halmashauri na shule umezingatia vigezo vifuatavyo; ukosefu wa mabweni kwa ajili ya jinsi zote, idadi ya wanafunzi wenyewe mahitaji maalum wanaosoma katika shule husika na umbali wa shule kutoka katika makazi ya wanafunzi hadi shulenii. Hivyo, baadhi ya shule zitajengewa mabweni mawili na nyingine bweni moja. Mgao wa mabweni haya kimkoa ni kama ulivyoonyeshwa katika **Kiambatisho namba 3**. Aidha mgao wa kila Halmashauri umeonyeshwa kwenye tovuti ya Ofisi ya Rais TAMISEMI; www.tamisemi.go.tz.

3.0 HUDUMA ZA AFYA YA MSINGI SHILINGI BILIONI 226.68

Kwa upande wa huduma za Afya Msingi, Vipaumbele vitakavyoteklezwa kuitia fedha hizi za Mpango wa Maendeleo kwa Ustawi wa taifa na mapambano dhidi ya UVIKO-19 ni;

- i. **Kuanzisha Huduma za Dharura “*Emergency Medical Department*” (EMD) katika Halmashauri 75 na kujenga majengo ya huduma za wagonjwa mahututi 25 katika Halmashauri 25 za kimkakati**

Serikali ya Rais Samia Suluhu Hassan katika mpango wake wa kuboresha huduma za afya nchini, inakwenda kujenga kwa mara ya kwanza majengo ya kutolea huduma za dharura (EMD) 75 kwenye maeneo ya kimkakati katika Halmashauri 75. Aidha,

Serikali itajenga majengo 25 ya wagonjwa mahututi katika Halmashauri 25 za kimkakati. Fedha hizi pia zitatumika kununulia Vifaa na Vifaa tiba vitakavyohitajika.

Vigezo vilivyozingatiwa katika ujenzi wa miundombinu ya huduma za dharura ni pamoja na maeneo yenyе sifa zifuatazo;

- a) Idadi kubwa ya watu;
- b) Maeneo yenyе umbali mrefu wa upatikanaji wa huduma za dharura;
- c) Maeneo yenyе milipuko ya magonjwa ya mara kwa mara na muingiliano mkubwa wa watu;
- d) Maeneo yenyе changamoto za ajali za mara kwa mara (*Barabara kuu*).

Mgao wa majengo ya wagonjwa wa dharura (EMD) na majengo ya vyumba vya wagonjwa mahututi (ICU) umeambatishwa kwenye **Kiambatisho namba 4 na 5**. Taarifa hii na pia kwenye tovuti ya Ofisi ya Rais - TAMISEMI; www.tamisemi.go.tz.

ii. Kusimika Mitambo 5 ya kufua Oksijeni na Mitambo 73 ya kusambaza Oksijeni Wodini

Ndugu Wanahabari

Serikali itajenga Mitambo 5 ya kuzalisha Oksijeni (*Oxygen Plant*) ambayo itapelekwa katika Halmashauri za Wilaya tano. Halmashauri hizo ni Karatu, Mlele, Bunda, Masasi na Nyasa ambapo kila Halmashauri imetengewa shilingi **milioni 600**. Aidha, Halmashauri hizi pia zitapata Mitambo 5 ya kusambaza Oksijeni wodini sambamba na Halmashauri nyingine 68 zilizopo kwenye maeneo yeye ajali hasa kwenye barabara kuu, maeneo yeye milipuko ya magonjwa ya mara kwa mara.

iii. Ununuzi wa Mitambo 60 Huduma ya Mionzi (Mashine za X-Ray)

Ndugu Wanahabari,

Fedha hizi pia zitatumika kununua mitambo 60 ya huduma za mionzi (machine za X-Ray) na kupelekwa kwenye maeneo ya mbali, idadi kubwa ya watu na maeneo yeye matukio ya ajali za mara kwa mara. Mgao wa mashine za mionzi (X-ray) umebainishwa kwenye **Kiambatisho namba 6**.

iv. Magari ya kubebea Wagonjwa (*Ambulances*) 195

Ndugu Wanahabari,

Serikali itanunua magari ya kubebea wagonjwa (*Ambulances*) 195 na kugawiwa katika Halmashauri zote 184. Halmashauri zinahimizwa kupelekwa ambulance hizi katika vituo vya afya vilivyo mbali sana kutoka katika Hospitali za Halmashauri ili kuwezesha huduma za rufaa kwa wagonjwa.

v. Magari ya usimamizi wa huduma za afya.

Serikali itanunua Magari 212 kwa ajili ya usimamizi na uratibu wa shughuli za Afya, Ustawi wa jamii na Lishe na usambazaji wa bidhaa za Afya katika Mikoa yote 26 na Halmashauri zote 184.

vi. Ujenzi wa Nyumba za Makazi ya watumishi wa Afya

Ndugu Wanahabari,

Katika hatua nyingine, Serikali itajenga nyumba **116** (zenye uwezo wa kuchukua familia 3) za watumishi wa afya na hivyo kuwezesha watumishi wa afya **348** kupata makazi ya uhakika. Vigezo vya maeneo ya ujenzi wa nyumba hizo ni pamoja na maeneo yaliyopo pembezoni hasa vituo vilivyo mbali na makao makuu ya Halmashauri, mbugani, visiwani, milimani na maeneo yenye changamoto za kufikika kirahisi. Kwa mantiki hii Halmashauri za Majiji, Manispaa na Miji hazikupewa kipaumbele kwenye mgao

huu. Mgao wa nyumba za watumishi wa afya umebainishwa kwenye **kiambatisho namba 7 cha Taarifa hii** na pia kwenye tovuti ya Ofisi ya Rais TAMISEMI. www.tamisemi.go.tz

vii. Ununuzi na Usambazaji wa Vifaa na VifaaTiba Mchanganyiko

Ndugu Wanahabari,

Serikali itanunua na kusambaza vifaa na vifaa tiba ikijumuisha vitanda na mashuka yake 2,208, mashine za usingizi sitini (60), taa za upasuaji sitini (60), majokofu ya kutunzia damu na mavazi kinga (PPE) kwa ajili ya wataalamu wetu.

**4.0 UWEZESHAJI WA WANANCHI KIUCHUMI SHILINGI
5,000,000,000.00**

Ndugu Wanahabari,

Serikali imepanga kuwezesha wafanyabiashara/wajasirimali wadogo kwa kuboresha mazingira ya kufanya biashara/shughuli zao wakiwemo wanawake, vijana na Watu Wenye Ulemavu. Jumla ya **shilingi billion 5** zimepangwa kutumika katika mpango huu, ambapo uchambuzi wetu umeonesha kuwa maeneo yenye wafanyabiashara wadogowadogo ni pamoja na Majiji ya Arusha, Dar es Salaam, Mbeya, Dodoma, Tanga, Mwanza na Manispaa za Ubungo, Kinondoni, Temeke na Morogoro.

Napenda kutumia nafasi hii kuwaelekeza Wakuu wa Mikoa na Wakuu wa Wilaya wahakikishe wanawasilisha andiko mahususi la maeneo yatakayoboreshwu kuitia mpango huu na kiasi cha fedha kinachokusudiwa kutumika kulingana na malengo ya Mpango huu. Taarifa hii iwasilishwe kwa maandishi kwangu kuitia Katibu Mkuu Ofisi ya Rais - TAMISEMI kabla ya tarehe **20 Oktoba, 2021**.

5.0 MAELEKEZO MAHSUSI KWA MIKO/WILAYA NA HALMASHAURI

Ndugu Wanahabari,

Napenda kutumia fursa hii kutoa maelekezo kwa Waheshimiwa Wakuu wa Mikoa na Wakuu wa Wilaya kusimamia mambo yafuatayo;

1. Kuunda Kamati ya Mkoa ya uratibu na ufuatiliaji wa utekelezaji wa miradi husika na kuhakikisha kwamba taarifa za utekelezaji wa miradi hii zinawasilishwa kwa Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais - TAMISEMI kila baada ya wiki mbili.
2. Kuhakikisha kila Halmashauri inaunda Kamati ya Halmashauri ya uratibu na ufuatiliaji wa utekelezaji wa miradi hii;
3. Kuhakikisha utekelezaji wa miradi unaanza ndani ya wiki mbili mara baada ya fedha kupokelewa;

4. Kuhakikisha Miradi ya ujenzi wa madarasa **inakamilika kabla au ifikapo tarehe 15 Desemba 2021** na Miradi mingine ikamilike **kabla au ifakapo tarehe 30/04/2022**;
5. Halmashauri zinaweza kutumia wakandarasi wa ndani au utaratibu wa "**force account**". Hata hivyo ninasisitiza gharama za utekelezaji kwa kutumia njia yoyote zisizidi makadirio ya fedha zilizotengwa kwa shughuli husika;
6. Halmashauri zitakazotaka kufanya mabadiliko ya utekelezaji wa eneo la mradi, maombi yawasilishwe kwa maandishi kwa Katibu Mkuu Ofisi Rais - TAMISEMI ndani ya wiki moja baada ya kupokea fedha hizo.
7. Ninaelekeza Viongozi wa Mikoa, Wilaya na Halmashauri katika kipindi hiki kuepuka safari zisizo za lazima zinazohusu kutoka nje ya Mkoa isipokuwa kwa kibali cha Viongozi Wakuu wa Nchi (Mhe Rais, Makamu wa Rais na Waziri Mkuu) ;
8. Utekelezaji wa miradi yote uzingatie Thamani ya fedha na ubora wa miradi;
9. Watoa huduma wa vifaa, mafundi watangaziwe kazi zilizopo kuitia tovuti za Mikoa, Halmashauri pamoja na mbao za matangazo katika ofisi za umma;
10. Halmashauri zinaelekezwa kufanya manunuzi ya pamoja (Bulk Procurement) ili kupunguza gharama za utekelezaji wa miradi;

11. Waheshimiwa Mameya na Wenyeviti wa Halmashauri pamoja na madiwani wote kupitia kamati zao wahakikishe wanasi mamia miradi hii kwa kushirikiana na watendaji wa Halmashauri;
12. Wakurugenzi wa Halmashauri wahakikishe miradi yote iliyokamilika na ununuzi wa vifaa zinawekwa alama ya **Mpango wa Maendeleo kwa Ustawi na Mapambano dhidi ya UVIKO-19.**
13. Kuhimiza wananchi kushiriki ujenzi wa miradi inayoendelea katika maeneo yao na kutoa taarifa endapo kuna ubadhirifu wa fedha.

Aidha, ninamuelekeza Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais - TAMISEMI kuwa na Kamati ya Wakurugenzi na Wakurugenzi Wasaidizi kwa ajili ya kuratibu utekelezaji wa Miradi hii na kuhakikisha fedha zinakwenda haraka. Kila Mkurugenzi na Mkurugenzi Msaidizi wa OR TAMISEMI apangiwe Mkoa mahususi kwa ajili ya kuratibu utekelezaji wa Miradi yote inayofanyika katika Mkoa.

Mwisho, Sambamba na fedha zilizopatikana kupitia Mpango huu wa **Maendeleo kwa Ustawi na Mapambano dhidi ya UVIKO-19,** Halmashauri zinaelekezwa kuendelea kusimamia mkakati wa ukusanyaji wa mapato ya ndani ya Halmashauri na kupeleka angalau asilimia 60 au 40 kwenye utekelezaji wa miradi ya maendeleo inayogusa wananchi moja kwa moja ikiwemo miradi ya

utoaji huduma za jamii katika sekta ya Elimu, Afya, miundombinu ya barabara na uwezeshaji wananchi kiuchumi. Nitumie nafasi hii kuwaelekeza Wakurugenzi wa Halmashauri zote nchini waendelee na ujenzi wa madarasa hususani kwa Shule za Msingi na kukamilisha ununuzi wa viti, meza pamoja na madawati katika vyumba vya madarasa ya zamani ili kujenga mazingira bora ya ufundishaji na ujifunzaji kwa watoto wetu nchini.

Mwisho kabisa napenda tena kumshukuru Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan kwa kufanikisha upatikanaji wa fedha hizi na kutupatia Ofisi ya Rais – TAMISEMI karibia nusu ya fedha zote zilizopatikana kwa ajili ya utekelezaji wa Miradi itakayotatua kero za wananchi wengi hususan wa Vijijini. Mheshimiwa Rais, tunaahidi kuwa tutasimamia kikamilifu fedha hizo ili ziweze kutekeleza kazi zote zilizopangwa.

“PAMOJA NA UVIKO-19 – KAZI IENDELEE”

Asanteni kwa kunisikiliza.



Ummy A. Mwalimu (Mb.)

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS – TAMISEMI

12 Oktoba, 2021

Jedwali Na. 1

**OFISI YA RAIS - TAMISEMI
MPANGO WA MAENDELEO KWA USTAWI WA TAIFA NA MAPAMBANO DHIDI YA UVIKO – 19**

MGAO WA VYUMBA VYA MADARASA KWA SHULE ZA SEKONDARI OKTOBA, 2021 KATIKA HALMASHAURI

MKOA	HALMASHAURI	MAHITAJI	VILIVYOPO	UPUNGUFU	MGAO	KIASI KWA DARASA	JUMLA YA FEDHA
Arusha	Arusha	178	82	96	96	20,000,000.00	1,920,000,000.00
	Arusha CC	233	128	105	105	20,000,000.00	2,100,000,000.00
	Karatu	103	45	58	58	20,000,000.00	1,160,000,000.00
	Longido	44	32	12	12	20,000,000.00	240,000,000.00
	Meru	142	72	70	70	20,000,000.00	1,400,000,000.00
	Monduli	71	35	36	36	20,000,000.00	720,000,000.00
	Ngorongoro	70	30	40	40	20,000,000.00	800,000,000.00
JUMLA NDOGO		841	424	417	417		8,340,000,000
Dar es Salaam	Ilala MC	543	288	255	255	20,000,000.00	5,100,000,000.00
	Kigamboni MC	83	49	34	34	20,000,000.00	680,000,000.00
	Kinondoni MC	271	125	146	146	20,000,000.00	2,920,000,000.00
	Temeke MC	389	232	157	157	20,000,000.00	3,140,000,000.00
	Ubungo MC	282	131	151	151	20,000,000.00	3,020,000,000.00
JUMLA NDOGO		1,568	825	743	743		14,860,000,000
Dodoma	Bahi	74	24	50	50	20,000,000.00	1,000,000,000.00
	Chamwino	126	44	82	82	20,000,000.00	1,640,000,000.00
	Chemba	98	33	65	65	20,000,000.00	1,300,000,000.00
	Dodoma CC	242	99	143	143	20,000,000.00	2,860,000,000.00
	Kondoa	91	41	50	50	20,000,000.00	1,000,000,000.00
	Kondoa TC	31	15	16	16	20,000,000.00	320,000,000.00
	Kongwa	165	53	112	112	20,000,000.00	2,240,000,000.00
	Mpwapwa	132	49	83	83	20,000,000.00	1,660,000,000.00
JUMLA NDOGO		959	358	601	601		12,020,000,000
Geita	Bukombe	118	54	64	64	20,000,000.00	1,280,000,000.00
	Chato	228	77	151	151	20,000,000.00	3,020,000,000.00
	Geita	462	115	347	347	20,000,000.00	6,940,000,000.00
	Geita TC	122	61	61	61	20,000,000.00	1,220,000,000.00
	Mbogwe	112	33	79	79	20,000,000.00	1,580,000,000.00
	Nyang'hwale	73	33	40	40	20,000,000.00	800,000,000.00

MKOA	HALMASHAURI	MAHITAJI	VILIVYOPO	UPUNGUFU	MGAO	KIASI KWA DARASA	JUMLA YA FEDHA
JUMLA NDOGO		1,115	373	742	742		14,840,000,000
Iringa	Iringa	142	76	66	66	20,000,000.00	1,320,000,000.00
	Iringa MC	79	46	33	33	20,000,000.00	660,000,000.00
	Kilolo	124	51	73	73	20,000,000.00	1,460,000,000.00
	Mafinga TC	42	26	16	16	20,000,000.00	320,000,000.00
	Mufindi	133	76	57	57	20,000,000.00	1,140,000,000.00
JUMLA NDOGO		520	275	245	245		4,900,000,000
Kagera	Biharamulo	136	45	91	91	20,000,000.00	1,820,000,000.00
	Bukoba	149	64	85	85	20,000,000.00	1,700,000,000.00
	Bukoba MC	68	38	30	30	20,000,000.00	600,000,000.00
	Karagwe	137	57	80	80	20,000,000.00	1,600,000,000.00
	KYERWA	133	48	85	85	20,000,000.00	1,700,000,000.00
	Missenyi	94	41	53	53	20,000,000.00	1,060,000,000.00
	Muleba	317	109	208	208	20,000,000.00	4,160,000,000.00
	Ngara	119	42	77	77	20,000,000.00	1,540,000,000.00
JUMLA NDOGO		1,153	444	709	709		14,180,000,000
Katavi	Mlele	17	7	10	10	20,000,000.00	200,000,000.00
	Mpanda	86	17	69	69	20,000,000.00	1,380,000,000.00
	Mpanda MC	77	29	48	48	20,000,000.00	960,000,000.00
	Mpimbwe	43	12	31	31	20,000,000.00	620,000,000.00
	Nsimbo	60	17	43	43	20,000,000.00	860,000,000.00
JUMLA NDOGO		283	82	201	201		4,020,000,000
Kigoma	Buhigwe	90	37	53	53	20,000,000.00	1,060,000,000.00
	Kakonko	68	22	46	46	20,000,000.00	920,000,000.00
	Kasulu	118	28	90	90	20,000,000.00	1,800,000,000.00
	Kasulu TC	96	39	57	57	20,000,000.00	1,140,000,000.00
	Kibondo	102	34	68	68	20,000,000.00	1,360,000,000.00
	Kigoma	112	43	69	69	20,000,000.00	1,380,000,000.00
	Kigoma/Ujiji MC	106	58	48	48	20,000,000.00	960,000,000.00
	Uvinza	152	34	118	118	20,000,000.00	2,360,000,000.00
JUMLA NDOGO		844	295	549	549		10,980,000,000
Moshi	Hai	89	46	43	43	20,000,000.00	860,000,000.00
	Moshi	188	103	85	85	20,000,000.00	1,700,000,000.00
	Moshi MC	70	48	22	22	20,000,000.00	440,000,000.00

MKOA	HALMASHAURI	MAHITAJI	VILIVYOPO	UPUNGUFU	MGAO	KIASI KWA DARASA	JUMLA YA FEDHA
Kilimanjaro	Mwanga	63	53	10	10	20,000,000.00	200,000,000.00
	Rombo	117	75	42	42	20,000,000.00	840,000,000.00
	Same	129	73	56	56	20,000,000.00	1,120,000,000.00
	Siha	42	24	18	18	20,000,000.00	360,000,000.00
JUMLA NDOGO		698	422	276	276		5,520,000,000
Lindi	Kilwa	106	32	74	74	20,000,000.00	1,480,000,000.00
	Lindi	59	21	38	38	20,000,000.00	760,000,000.00
	Lindi MC	62	27	35	35	20,000,000.00	700,000,000.00
	Liwale	41	15	26	26	20,000,000.00	520,000,000.00
	Nachingwea	87	30	57	57	20,000,000.00	1,140,000,000.00
	Ruangwa	52	19	33	33	20,000,000.00	660,000,000.00
JUMLA NDOGO		407	144	263	263		5,260,000,000
Manyara	Babati	135	57	78	78	20,000,000.00	1,560,000,000.00
	Babati TC	39	23	16	16	20,000,000.00	320,000,000.00
	Hanang	115	47	68	68	20,000,000.00	1,360,000,000.00
	Kiteto	71	27	44	44	20,000,000.00	880,000,000.00
	Mbulu	69	30	39	39	20,000,000.00	780,000,000.00
	Mbulu TC	48	28	20	20	20,000,000.00	400,000,000.00
	Simanjiro	39	27	12	12	20,000,000.00	240,000,000.00
JUMLA NDOGO		516	239	277	277		5,540,000,000
MARA	BUNDA	116	49	67	67	20,000,000.00	1,340,000,000.00
	Bunda TC	92	41	51	51	20,000,000.00	1,020,000,000.00
	Butiama	117	45	72	72	20,000,000.00	1,440,000,000.00
	Musoma	108	41	67	67	20,000,000.00	1,340,000,000.00
	Musoma MC	73	56	17	17	20,000,000.00	340,000,000.00
	Rorya	165	67	98	98	20,000,000.00	1,960,000,000.00
	Serengeti	160	58	102	102	20,000,000.00	2,040,000,000.00
	Tarime	176	60	116	116	20,000,000.00	2,320,000,000.00
	Tarime TC	57	29	28	28	20,000,000.00	560,000,000.00
JUMLA NDOGO		1,064	446	618	618		12,360,000,000
Mbeya	Busokelo	55	31	24	24	20,000,000.00	480,000,000.00
	Chunya	68	23	45	45	20,000,000.00	900,000,000.00
	Kyela	130	63	67	67	20,000,000.00	1,340,000,000.00
	Mbarali	147	53	94	94	20,000,000.00	1,880,000,000.00

MKOA	HALMASHAURI	MAHITAJI	VILIVYOPO	UPUNGUFU	MGAO	KIASI KWA DARASA	JUMLA YA FEDHA
	Mbeya	156	64	92	92	20,000,000.00	1,840,000,000.00
	Mbeya CC	207	120	87	87	20,000,000.00	1,740,000,000.00
	Rungwe	128	73	55	55	20,000,000.00	1,100,000,000.00
JUMLA NDOGO		891	427	464	464		9,280,000,000
Morogoro	Gairo	80	25	55	55	20,000,000.00	1,100,000,000.00
	Ifakara TC	118	63	55	55	20,000,000.00	1,100,000,000.00
	Kilombero	112	34	78	78	20,000,000.00	1,560,000,000.00
	Kilosa	222	75	147	147	20,000,000.00	2,940,000,000.00
	Malinyi	54	20	34	34	20,000,000.00	680,000,000.00
	Morogoro	147	44	103	103	20,000,000.00	2,060,000,000.00
	Morogoro MC	177	91	86	86	20,000,000.00	1,720,000,000.00
	Mvomero	157	50	107	107	20,000,000.00	2,140,000,000.00
	Ulanga	72	30	42	42	20,000,000.00	840,000,000.00
JUMLA NDOGO		1,139	432	707	707		14,140,000,000
Mtwara	Masasi	118	34	84	84	20,000,000.00	1,680,000,000.00
	Masasi TC	52	17	35	35	20,000,000.00	700,000,000.00
	Mtvara	71	21	50	50	20,000,000.00	1,000,000,000.00
	Mtvara Mikindani	53	31	22	22	20,000,000.00	440,000,000.00
	Nanyamba TC	46	15	31	31	20,000,000.00	620,000,000.00
	Nanyumbu	75	17	58	58	20,000,000.00	1,160,000,000.00
	Newala	49	22	27	27	20,000,000.00	540,000,000.00
	Newala TC	40	21	19	19	20,000,000.00	380,000,000.00
	Tandahimba	119	37	82	82	20,000,000.00	1,640,000,000.00
JUMLA NDOGO		623	215	408	408		8,160,000,000
Mwanza	Buchosa	189	61	128	128	20,000,000.00	2,560,000,000.00
	Ilemela MC	217	120	97	97	20,000,000.00	1,940,000,000.00
	Kwimba	182	73	109	109	20,000,000.00	2,180,000,000.00
	Magu	193	70	123	123	20,000,000.00	2,460,000,000.00
	Misungwi	207	61	146	146	20,000,000.00	2,920,000,000.00
	Mwanza CC	244	146	98	98	20,000,000.00	1,960,000,000.00
	Sengerema	204	75	129	129	20,000,000.00	2,580,000,000.00
	Ukerewe	219	64	155	155	20,000,000.00	3,100,000,000.00
JUMLA NDOGO		1,655	670	985	985		19,700,000,000
		Ludewa	75	28	47	20,000,000.00	940,000,000.00

MKOA	HALMASHAURI	MAHITAJI	VILIVYOPO	UPUNGUFU	MGAO	KIASI KWA DARASA	JUMLA YA FEDHA
Njombe	Makambako TC	58	32	26	26	20,000,000.00	520,000,000.00
	Makete	46	24	22	22	20,000,000.00	440,000,000.00
	Njombe	45	21	24	24	20,000,000.00	480,000,000.00
	Njombe TC	69	32	37	37	20,000,000.00	740,000,000.00
	Wanging'ombe	82	46	36	36	20,000,000.00	720,000,000.00
JUMLA NDOGO		375	183	192	192		3,840,000,000
Pwani	Bagamoyo	68	31	37	37	20,000,000.00	740,000,000.00
	Chalinze	115	49	66	66	20,000,000.00	1,320,000,000.00
	Kibaha	40	20	20	20	20,000,000.00	400,000,000.00
	Kibaha TC	90	43	47	47	20,000,000.00	940,000,000.00
	Kibiti	75	24	51	51	20,000,000.00	1,020,000,000.00
	Kisarawe	62	25	37	37	20,000,000.00	740,000,000.00
	Mafia	24	12	12	12	20,000,000.00	240,000,000.00
	Mkuranga	166	50	116	116	20,000,000.00	2,320,000,000.00
	Rufiji	58	22	36	36	20,000,000.00	720,000,000.00
JUMLA NDOGO		698	276	422	422		8,440,000,000
Rukwa	Kalambo	85	26	59	59	20,000,000.00	1,180,000,000.00
	Nkasi	109	41	68	68	20,000,000.00	1,360,000,000.00
	Sumbawanga	118	31	87	87	20,000,000.00	1,740,000,000.00
	Sumbawanga MC	105	60	45	45	20,000,000.00	900,000,000.00
JUMLA NDOGO		417	158	259	259		5,180,000,000
Ruvuma	Madaba	27	10	17	17	20,000,000.00	340,000,000.00
	Mbinga	128	40	88	88	20,000,000.00	1,760,000,000.00
	Mbinga TC	57	23	34	34	20,000,000.00	680,000,000.00
	Namtumbo	112	32	80	80	20,000,000.00	1,600,000,000.00
	Nyasa	71	27	44	44	20,000,000.00	880,000,000.00
	Songea	69	23	46	46	20,000,000.00	920,000,000.00
	Songea MC	83	57	26	26	20,000,000.00	520,000,000.00
	Tunduru	145	32	113	113	20,000,000.00	2,260,000,000.00
JUMLA NDOGO		692	244	448	448		8,960,000,000
Shinyanga	Kahama TC	152	57	95	95	20,000,000.00	1,900,000,000.00
	Kishapu	129	48	81	81	20,000,000.00	1,620,000,000.00
	Msalala	104	35	69	69	20,000,000.00	1,380,000,000.00
	Shinyanga	109	44	65	65	20,000,000.00	1,300,000,000.00

MKOA	HALMASHAURI	MAHITAJI	VILIVYOPO	UPUNGUFU	MGAO	KIASI KWA DARASA	JUMLA YA FEDHA
	Shinyanga MC	79	44	35	35	20,000,000.00	700,000,000.00
	Ushetu	76	28	48	48	20,000,000.00	960,000,000.00
JUMLA NDOGO		649	256	393	393		7,860,000,000
Simiyu	Bariadi	76	32	44	44	20,000,000.00	880,000,000.00
	Bariadi TC	76	34	42	42	20,000,000.00	840,000,000.00
	Busega	141	51	90	90	20,000,000.00	1,800,000,000.00
	Itilima	109	31	78	78	20,000,000.00	1,560,000,000.00
	Maswa	128	58	70	70	20,000,000.00	1,400,000,000.00
	Meatu	83	27	56	56	20,000,000.00	1,120,000,000.00
JUMLA NDOGO		613	233	380	380		7,600,000,000
Singida	Ikungi	116	49	67	67	20,000,000.00	1,340,000,000.00
	Iramba	84	37	47	47	20,000,000.00	940,000,000.00
	Itigi	44	15	29	29	20,000,000.00	580,000,000.00
	Manyoni	74	26	48	48	20,000,000.00	960,000,000.00
	Mkalama	74	27	47	47	20,000,000.00	940,000,000.00
	Singida	108	50	58	58	20,000,000.00	1,160,000,000.00
	Singida MC	74	40	34	34	20,000,000.00	680,000,000.00
